## *UTANGULIZI*

Parachichi, kitaalamu *Persea Americana* ni tunda lenye virutubisho muhimu sana vinavyohitajika katika mwili wa binadamu na linaongeza kipato kwa familia na Taifa.

## *AINA ZA PARACHICHI*

### A: Parachichi za Asili

Parachichi za asilia miti yake huwa ni mirefu sana na mavuno yake ni machache.

### B: Aina za Kisasa/Chotara

**1. Hass**, Sifa kuu-lina vipere vipere sehemu ya juu ya ganda/ngozi yake, huchukua miezi 10-14 maeneo ya baridi kukomaa), uzito wa tunda ni gramu 150-300.





*Parachichi aina ya Hass*

**2. Fuerte:**

Ni aina ya chotara inayotokana na mchanganyiko wa aina za Guatemala na Mexico Sifa kuu lina ngozi nyembamba na laini. Hukomaa baada ya miezi 4-6 tangu mti wake ulipotoa maua na uzito wa tunda ni gramu 230-500.



*Parachichi aina ya Fuerte*

**3. X-Ikulu.**

Aina hii ni maarufu sana kwa mikoa ya nyanda za juu kusini (Njombe, Iringa, Mbeya na Ruvuma). Kiumbo tunda lake ni kubwa, majani yake ni mapana kama mti wa embe, rangi ya ganda ni kijani kabla na baada ya kuiva. Huchukua miezi sita kutoka maua hadi kukomaa na hukomaa wakati aina nyingine hazipo sokoni.



*Parachichi aina ya X-Ikulu*

## *SEHEMU YA KUPANDA*

Panda sehemu zenye udongo usiotuamisha maji na wenye rutuba kuepuka magonjwa ya mizizi. Parachichi hustawi vizuri katika maeneo yenye mwinuko wa mita 1,500 – 2,100 kutoka usawa wa bahari na wastani wa mvua za mm 1,000 zenye mtawanyiko mzuri. Joto linalofaa ni kati ya $25^{0}C$ – $30^{o}C$

## *UPANDAJI*

**Nafasi ya upandaji**:

Nafasi kati ya shimo na shimo na mstari kwa mstari kwa ekari moja (1) yaweza kuwa:

- Mita 7 x 7 (miche 80 mpaka 85)
- Mita 8 x 8, (miche 60 mpaka 65)
- Mita 4x 8 (miche 125 mpaka 128) kutegemeana na aina ya parachichi.

**Ukubwa wa shimo**:

Shimo linashauriwa kuwa na ukubwa wa futi 3 x futi 3 x futi 3 (upana x urefu x kina). Mashimo yaandaliwe mapema miezi 2 mpaka 3 kabla ya kupanda miche shambani. Wakati wa uchimbaji tenganisha udongo wa juu na chini.

**Umwagiliaji:**

Ni muhimu kumwagilia miche ya parachichi ili kuongeza uzalishaji. Wakati wa kiangazi mwagilia angalao mara mbili kwa mwezi.

### *MBOLEA*

Unaweza kutumia mbolea za asili (Samadi, Mboji) au za viwandani (DAP, Minjingu, NPK au TSP). Weka Samadi au Mboji, kilo 16 hadi 20 kwa shimo, mwezi moja kabla ya kupanda. Kwa mbolea za viwandani weka gramu 100 hadi 200 kwa shimo. Zingatia kuchanganya vizuri mbolea na udongo.

### *KUDHIBITI MAGUGU*

Hakikisha shamba linakuwa safi wakati wote ili kuongeza uzalishaji maana magugu yanakula chakula cha mimea na ni chanzo cha magonjwa, yadhibiti kwa kutumia jembe au kwanja, au tumia viua gugu. (yenye viambata vya glyphosate).

### *MAGONJWA NA WADUDU*

Parachichi hushambuliwa na magonjwa kama mimea mingine hasa kwa upande wa majani na matunda. Magonjwa hayo husababishwa na fangasi/ ukungu, Algae, wadudu pamoja na lishe duni ya mmea.

### *UDHIBITI -MAGONJWA NA WADUDU*

**Kudhibiti wadudu**:

Ili kudhibiti wadudu tumia viuatilifu kama vile lambdacyhalothrin, deltamethrin na emamectin benzoate.

**Kudhibiti Ukungu:**

Kwa matatizo ya ukungu, tumia viuatilifu vyenye viambata vyenye mancozeb na metalax.

### UVUNAJI

Parachichi zilizobebeshwa hukomaa baada ya miaka miwili na nusu mpaka mitatu. Mambo ya kuzingatia: Vuna kwa wakati, weka kwenye ndoo za plastiki/kreti. Usivune wakati wa mvua/umande kuepuka kuoza. Hakikisha kikonyo kinabaki kwenye tunda.



**Mavuno:** mti bora wa parachichi wenye miaka 4-5 huweza kuzaa matunda 300 – 400 kwa mwaka na mti wenye miaka 7 na kuendelea huzaa matunda 800 hadi 1,000 kwa mwaka. Aina ya HASS inauzwa kati ya Tshs.1000 hadi 1500 kwa kilo (mwaka 2020). Kilo moja inaingia parachichi 3 hadi 4.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

**MENEJA,**
***TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO,***
***TARI KIFYULILO,***
***S.L.P 93 MUFINDI,***
***SIMU: 0765176040/0769492549,***
***Baruapepe: cmkifyulilo@tari.go.tz, Tovuti: www.tari.go.tz***

# TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA (TARI)

TARI
Transforming Agriculture

## ZALISHA PARACHICHI KIBIASHARA



